TANGAZO LA SERIKALI NA. 946 la tarehe 29/11/2019

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA,
(NA. 5 YA MWAKA 2019)

AGIZO

(Imetolewa kwa mujibu wa Kifungu Na.29(1)(d))

AGIZO LA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA NANSIO (NANSIO WSSA), LA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA), 2019

Jina la Agizo

1. Agizo hili litajulikana kama, Agizo la Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Nansio(Nansio WSSA), (Kurekebisha Bei za Huduma za Maji safi na Usafi wa Mazingira), la Mwaka 2019.

Tarehe ya Kuanza kutumika

2. Agizo hili litaanza kutekelezwa rasmi kuanzia tarehe 1 Disemba 2019.

Marekebisho ya Bei

3. Bei za majisafi na usafi wa mazingira za Nansio WSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza katika Agizo hili.

Masharti

4. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:

(a) kabla ya kuanza kutekeleza bei mpya, Nansio WSSA iwasilishe EWURA vielelezo kwamba ilitoa taarifa kwa wateja wake kuhusu bei mpya za huduma zake na pia ilitoa elimu kikamilifu kwa umma ikiwa ni pamoja na wawakilishi wa wananchi, serikali na viongozi wa dini katika eneo lake la huduma;

(b) Nansio WSSA ihakikishe inanunua na kuweka stoo dira za kutosha kwa ajili ya kubadilisha zilikwisha muda wake ili zoezi la ubadilishwaji wa dira lifanyike kwa kipindi kifupi;

(c) Ifikapo tarehe 31 Januari2020 au kabla, Nansio WSSA itawasilisha EWURA mpango wake wa kibiashara (2019/20-2021/22) uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango

wa utekelezaji wa masharti ya Agizo hili;

(d) Nansio WSSA, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Agizo hili;

(e) Nansio WSSA itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la Agizo hili;

Sura 414

T.S. Na 193 la mwaka 2010

(f) Nansio WSSA itatekeleza kifungu cha 43 cha Sheria ya EWURA na Kanuni ya sita (6) ya EWURA ya Kanuni u za Kukusanya Ada na Tozo zilizochapishwa katika Tangazo la Serikali la mwaka 2010;

Sura 348

(g) Nansio WSSA itahakikisha ripoti zake za kifedha zinakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali au taasisi yeyote ya ukaguzi wa fedha iliyoidhinishwa kama kifungu cha 33 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Hesabu za Umma na kupeleka nakala za taarifa za kifedha zilizokaguliwa kwa EWURA-

(h) Ifikapo tarehe 31 Desemba 2019 au kabla Nansio WSSA iandae na kuwasilisha EWURA mpango wa kuwafikia wateja wake kwa lengo la kutoa elimu juu ya Huduma za maji;

(i) Nansio WSSA, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Agizo la Bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Nne la Agizo hili; na

(j) Nansio WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Nansio WSSA ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za majisafi na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa huduma zake. Pia EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na Nansio WSSA katika siku zijazo.

Utenguzi wa Agizo T.S Na. 453 la mwaka 2017

5. Agizo hili linatengua Agizo lililochapishwa kwente Tangazo la Serikali la mwaka 2017.

MAJEDWALI

JEDWALI LA KWANZA

(Limetengenezwa chini ya aya ya 3)

BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali 1.1: Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi/ Mita ya Ujazo)

Kundi la Wateja	Bei ya Sasa	Bei Zilizoidhinishwa		
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani	725	1,090	1,370	1,460
Taasisi	840	1,260	1,460	1,530
Biashara	1,180	1,500	1,600	1,620
Viwanda	1,415	1,600	1,650	1,660
Magati	1,200	1,250	1,300	1,400
Ujenzi	-	1,305	2,000	2,500
Wastani	831	1,325	1,381	1,466

Jedwali 1.2: Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Maunganisho Mapya (TZS/Unganisho)

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Iliyoidhinishwa		
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani Taasisi Biashara Viwanda Ujenzi Viwanda vya Maji ya Chupa	Asilimia 20 ya Gharama za Maunganisho kama ilivyoelezwa katika Kanuni za Maji za Mwaka 2013	Asilimia 20 ya Gharama za Maunganisho kama ilivyoelezwa katika Kanuni za Maji za Mwaka 2013		

Jedwali 1.3: Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Marejesho ya Huduma ya Maji Baada ya Kukatiwa (TZS/Rejesho)

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Zilizoidhinishwa		
	2018/19			
Majumbani	12,000	15,000	15,000	15,000
Taasisi	30,000	15,000	15,000	15,000
Biashara	30,000	15,000	15,000	15,000
Viwanda	40,000	15,000	15,000	15,000
Magati	20,000	15,000	15,000	15,000
Ujenzi	-	15,000	15,000	15,000

Jedwali 1.4: Tozo ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Kuondoa Majitaka (TZS/Gari)

TANGAZO LA SERIKALI NA. 946 (linaendelea)

Kundi la Wateja	Uwezo wa Gari (m^3)	Tozo ya Sasa	Tozo Zilizoidhinishwa		
		2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Wateja Wote	1-3	104,000	70,000		
	4-6	104,000	90,000		
	7-9	104,000	120,000		
	≥10	104,000	130,000		

JEDWALI LA PILI

(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(d))

MIRADI ITAKAYOTOKELEZWA (SHILINGI MILIONI)

Maelezo ya Kazi Zitakazofanyika	2019/2020	2020/2021	2021/2022
Kununua Dira za Maji 3,000 za ¾" kwa ajili ya wateja wapya	50.00	60.00	72.00
Kununua vifaa vya kutendea kazi (Machine ya kuunganishia mabomba, machine ya kuungia vyuma, spana ya fundibomba, sepetu, jembe, jambeni, grisi n.k)	79.00	41.00	30.00
Kununua vifaa vya maabara, zana na madawa	100.00	160.00	180.00
Kununua pikipiki 5 na baiskeli 10P			17.40
Kununua Samani za ofisini (Viti 10,Meza 3 na Makabati 2)		7.60	
Kununua Kompyuta 4 Printa 2 na vifaa vyake	14.00		
Kununua na kufunga mtambo wa umeme jua kwenye Matangi ya Nabuye na Malegea	10.00		
Kuweka mfumo wa komyuta wa kutolea Ankara za maji		40.00	
Kujenga Magati ya maji 15	30.00	45.00	50.00

TANGAZO LA SERIKALI NA. 946 (linaendelea)

Maelezo ya Kazi Zitakazofanyika	2019/2020	2020/2021	2021/2022
Kuongeza Mtandao wa Maji hadi Malegea, Bukongo, Kakerege, Nakatunguru, Nkilizya, Bulamba, Hamkoko, Nebuye, Butiriti, Nantare, Nansio na Muruseni km 61.5 (DN 25 – DN 160).	100.00	395.00	230.00
Kukarabati km 1.5 za njia kuu ya maji (DN 160) na km 4 za bomba la kusambaza maji (DN 75-DN 125) maeneo ya Nkilizya, Nansio na Nakatunguru	-	70.00	149.58
Kukarabati tangi la maji, jingo na chemba ya maji Nabuye, Malegea, Nansio na kwenye bwawa la maji taka Hamkoko	-	50.00	100.42
Kununua Dira za Maji 750 kwa ajili ya kubadilisha	12.00	15.00	18.00
Kukarabati magari matatu, pkipiki tatu na baiskeli kumi	35.00	35.00	35.00
Jumla ya Gharama za Uwekezaji	430.00	918.60	882.40

JEDWALI LA TATU

(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(e))

VIASHIRIA VYA UTENDAJI (2019/20 – 2021/22)

Maelezo	Kipimo	Lengo la Utendaji		
		2019/20	2020/21	2021/22
Idadi ya wateja wapya wa maji safi	Na	600	600	600
Kiwango cha upotevu wa maji	%	28	26	25
Wateja wenye Dira	%	100	100	100
Kiwango cha ufanisi katika ukusanyaji wa mapato	%	90	90	95

JEDWALI LA NNE

(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(i))

MAHITAJI YA FEDHA YALIYOIDHINISHWA (SHILINGI MILIONI)

MAELEZO	2019/20	2020/21	2021/22
Uzalishaji wa Maji	352.40	440.05	516.63
Usambazaji	65.00	77.00	152.00
Uondoaji Majitaka	25.88	38.25	66.63
Matengenezo	45.00	67.00	98.00
Watumishi	141.05	149.00	158.00
Utawala	63.20	53.20	65.90
Matangazo	28.50	39.20	48.50
Matukio	8.50	10.50	17.50
Bodi	23.50	30.35	36.50
Benki	0.00	0.00	0.00
Jumla (Uendeshaji na Matengenezo	753.02	904.55	1,159.65
Uchakavu	374.08	423.59	480.03
Uwekezaji	178.16	470.69	614.83
Jumla ya Mahitaji ya Fedha	1,305.27	1,798.83	2,254.51
Ondoa: Ruzuku	53.53	53.53	53.53
Ondoa: Mapato yasiyo ya Maji	25.18	26.02	25.14
Jumla ya Mahitaji ya Fedha Kutokana na Mauzo ya Maji	1,226.56	1,719.28	2,175.85
Kiasi cha Maji Yatakayozalishwa (Mil. m^3)	1.29	1.68	1.98
Upotevu wa Maji (%)	28%	26%	25%
Kiasi cha Maji Yatakayouzwa (Mil. m^3)	0.93	1.25	1.49
Wastani wa Bei (TZS/m^3)	1,324	1,380	1,465

Dodoma
14 Novemba, 2019

NZINYANGWA E. MCHANY
Mkurugenzi Mkuu